# IGUNGA YA MAENDELEO

## DC IGUNGA AWAFUNDA WATENDAJI WA KATA 9 WALIOKABIDHIWA PIKIPIKI



Mkuu wa wilaya ya Igunga Tabora amewataka watendaji wote wa kata kwenda kutekeleza majukumu yao kwa wakati na weledi,
Amewaambia watendaji hao kuwa lengo la kupewa pikipiki ni kuwahudumia wananchi, hategemei kuona pikipiki hizo zikabadilishiwa matumizi kinyume na malengo ya serikali.
Aidha DC Ameupongeza uongozi Mzuri wa Mkurugenzi mtendaji bi Fatuma Latu, kwa kuitumia chenji iliobaki kwenye ununuzi wa gari na kuamua kufanya kitu kinachoonekana.

# DED IGUNGA: CHENJI IKIBAKI TUNAFANYIA MAMBO YA MAANA



“Mh. Mkuu wa wilaya tulipewa fedha na mheshimiwa Rais mama Samia suluhu Hasani,ya kununulia gari la mkurugenzi mtendaji wilaya ya igunga,Fedha zilizobaki(chenji) tukakubaliana katika vikao halali, kununua pikipiki 11 ambazo leo utazigawa kwa watendaji wa kata 9, pikipiki 1 atapewa mwandishi wa vikao (cc) na nyingine itakuwa kitengo cha fedha"

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya igunga, Bi Fatuma Omari Latu, wakati wa kumkaribisha Mkuu wa wilaya Mheshimiwa Sauda Mtondoo kwenye hafla fupi ya kukabidhi pikipiki hizo.

# SHERIA NA TARATIBU ZA NCHI ZIFUATWE

Mkuu wa wilaya igunga, Amewataka watendaji wa kata 9 waliopewa pikipiki tarehe 14/7/2022 wahakikishe wanapata mafunzo ya kuendesha pikipiki, mafunzo ya usalama barabarani na kupata leseni, Nchi hii inaendeshwa kwa sheria. (alisema DC).Lakini pia mafunzo yanakufanya uwe salama wewe mwenyewe, watumiaji wa



barabara, na chombo chenyewe pia kitadumu.

## WATENDAJI WA KATA KUMEKUCHA KUHUDUMIA WANANCHI.

**Baada ya kukabidhiwa pikipiki makao makuu ya wilaya ya igunga sasa wanaelekea kwenye kata zao kuchapa kazi.**



Watendaji wa Kata 9 baada ya kukabidhiwa pikipiki, zilizonunuliwa kwa fedha iliyobaki (chenji) baada ya kununua gari jipya la mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya igunga

## AFISA MTENDAJI WA KATA YA KINUNGU AISHUKURU SERIKALI



Afisa mtendaji wa kata ya Kinungu, Bw Michael Leonard Myampi, ameishukuru serikali ya mama Samia Suluhu Hasani, kwa mambo mazuri yanayofanyika kwa wananchi,

pia ameushukuru uongozi wa halmashauri na uongozi wa Bi Fatuma Latu kwa kuwafikiria na kuwapa vyombo vya usafiri(pikipiki) “Tunaahidi kuwa tutatekeleza majukumu yetu kama yalivyoainishwa kwenye muongozo, ni rahisi kufika kila kijiji katika kata na kusimamia shughuli za maendeleo katika kata” *Alisema Michael Leonard Mtendaji wa kata ya Kinungu.*

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa